# TUMEAMUA, TUNATEKELEZA
# TAARIFA YA UTEKELEZAJI

Na. Dkt. Hassan Abbasi, Msemaji Mkuu wa Serikali

DODOMA, 30 JANUARI, 2020.

# UTANGULIZI

- **1.SALAAM ZA MWAKA MPYA**: Kwa kuwa leo ni Mkutano wangu wa kwanza na wanahabari kwa mwaka huu, nianze kwa kutoa salaam za Mwaka Mpya 2020 kwenu na kwa Watanzania wote;

- **2. UTOAJI WA PRESS CARD**: **Napenda pia kuwajulisha wanahabari kuwa** tumeanza kutoa PRESS CARDS katika ofisi zetu za Dar na Dodoma na Ofisi za Maafisa Habari nchi nzima. Ifikapo Februari 29, 2020, hakuna mwanahabari atashiriki shughuli za umma bila kadi hii; na

- **3. MKUTANO MBEYA**: Mkutano wa Maafisa Habari/Wasemaji wa Serikali kufanyika Mbeya, Machi 9 mpaka 13, 2020. Natumia nafasi hii kuwakumbusha viongozi kutekeleza maagizo ya Waziri Mkuu kwa kuwaruhusu na kuwawezesha maafisa habari waje wafundwe zaidi katika kazi yao.

# MUHTASARI

- **Taarifa ya leo itajikita katika:**
- **1. Tanzania Kimataifa:** Rushwa na Utalii;
- **2. Hali ya Uchumi:** Mwenendo wa Uchumi, Mapato ya Serikali;
- **3. Mageuzi ya Rais Magufuli Yanaendelea Kulipa:** Rekodi ya Mapato, Rekodi ya Madini, Rekodi ya Utoaji wa Fedha kwa Miradi/Ofisi za umma; na
- 
- **4. Maswali na Majibu:** Kujibu maswali ya waandishi

# TANZANIA KATIKA UGA WA KIMATAIFA

**1. RUSHWA: Ripoti ya Transparency 2019 ya Januari 23, 2020:** Tanzania imekuwa ya 96 kutoka ya **117 mwaka 2015 na 103 mwaka 2017.** Haya ni mageuzi makubwa. Kwa matokeo haya Tanzania ni ya pili kwa Afrika Mashariki kwa kutokuwa na rushwa nyuma ya Rwanda;

Aidha mtakumbuka kuwa katika kipengele cha juhudi za kupambana na rushwa, Julai mwaka jana Tanzania iliongoza takribani nchi 15 za Afrika zilizofanyiwa utafiti na taasisi za Transparency na Afrobaramoter.

Haya ni mafanikio ya msimamo wa Rais Magufuli, mageuzi ya kimfumo na kitaasisi aliyoyafanya ikiwemo kuanzisha Mahakama ya Mafisadi na kuchukua hatua haraka hasa yanapotendeka makosa ya uhujumu uchumi.

# TANZANIA KATIKA UGA WA KIMATAIFA

- **2. UTALII**: Miaka mitatu iliyopita tuliimarisha mifumo ya kodi, watu wakatishia kuwa watalii watakimbia nchini. Wameongezeka zaidi. Ripoti ya Taasisi maarufu za Utalii ya mwishoni mwa mwaka jana, imeonesha kuwa kwa mwaka 2018 Tanzania imekuwa ya nne Afrika kwa kuingiza mapati ya utalii ikitanguliwa na Afrika Kusini, Misri na Moroko [Iliingiza Dola za Marekani Bilioni 2.43 kutoka Dola Bilioni 2.19 mwaka 2017.

- **2. CNNTravel**: CNN katika taarifa ya Novemba, 2019, “Africa’s Most Amazing Places To Visit in 2020” Tanzania imekuwa namba moja [Hifadhi ya Serengeti]. Nchi yetu ni ya pekee na dunia inajua.

# HALI YA UCHUMI; TANZANIA

Wakati taarifa ya IMF ya Januari 20, 2020 ikionesha kuwa Uchumi wa Dunia utakua kidogo kutoka ukuaji wa asilimia 2.9 hadi asilimia 3.3 kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20 [Julai-Disemba, 2019] uchumi wa Tanzania umeendeleaa kuwa imara kwa kukua kwa asiliamia 6.9 kwa takwimu za mpaka Septemba, 2019 (lengo ni kwenda mpaka 7.0 na 7.1%). Huu ni ukuaji mkubwa katika nchi za Afrika Mashariki nyuma ya Rwanda pekee na bado tuko miongoni mwa nchi za juu kwenye ukanda wa SADC na Afrika kwa ujumla;

Sekta zilizochangia sana ukuaji huo ni: *Ujenzi (16%); uchimbaji madini na mawe (13.7%), habari na mawasiliano (10.7%), maji (9.1%) na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (9.0%).*

# MAAMUZI MAGUMU YANALIPA; MAFANIKIO LUKUKI

- Moja ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kusimamia mifumo ya kimageuzi ambayo sasa imeanza kuleta mafanikio makubwa na ya kihistoria nchini;

- Katika eneo hili tutaangalia mafanikio katika: Ukusanyaji wa mapato na jinsi uchumi unavyozidi kuchangamka kwa mauzo ya bidhaa muhimu kwenda nje kuzidi kuongezeka ikiakisi mageuzi muhimu ambayo Rais Magufuli ameyafanya nchini.

# REKODI MPYA YA UKUSANYAJI MAPATO

- *Ndugu wanahabari;*

- Kwa miaka mitatu sasa habari kubwa katika mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano katika ukusanyaji wa mapato kwa mwezi ilikuwa ni kutoka TZS Bilioni 850 mwaka 2015 hadi TZS Trilioni 1.3;

- Leo ninayo furaha kulitangazia rasmi Taifa kuwa kutokana na juhudi kubwa zilifanywa na Serikali kupitia TRA na Idara nyingine za Serikali, wastani wa mapato ya kodi kwa mwezi kati ya Julai-Disemba, 2019, UMEPANDA na sasa ni TZS Trilioni 1.5 kwa mwezi. Hii kwa sasa ndio rekodi mpya, na ndio habari mpya ya mjini. TUMEAMUA na Safari ya KUTEKELEZA inaendelea na uwezo wetu wa kuhudumia sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi umezidi KUIMARIKA.

# MADINI; MAUZO NJE YAONGEZEKA

- **Taarifa ya BoT Novemba, 2019**: Takwimu zinaonesha kuwa mauzo ya bidhaa zisizo kuwa zile za kawaida yameongezeka kwa asilimia 31.0 kwa sababu kubwa mbili muhimu:

- **1. Kuongezeka mauzo ya dhahabu**: Wote mnafahamu kuwa Serikali imechukua hatua kubwa kuanzisha masoko ya madini na kuzuia uuzaji holela na utoroshaji wa madini. Matokeo yake tumeanza kufaidi. Hadi Novemba, 2019, mauzo ya dhahabu nje ambayo ni asilimia 51.4 ya mauzo yote ya bidhaa nje ya nchi (bidhaa zisizo za kawaida, yaliongezeka kwa asilimia 41.9 kufikia kiasi cha Dola Bilioni 2.1;

- **Viwanda vyaleta matokeo makubwa**: Aidha sera ya kuchagiza ujenzi wa viwanda nayo imezidi kulipa. Mauzo ya bidhaa za viwandani nje yameongezeka kwa asilimia 28.4 kufikia Dola milioni 996.0 ikichangiwa zaidi na bidhaa kama bidhaa za chuma na mabati, vioo, tumbaku, katani na mbolea.

# SHUKRANI KWA KUSHIRIKI